Kijarida Kuhusu

KASHFA

Kimeandaliwa na:

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

© LHRC

Septemba, 2013

Yaliyomo

SHUKURANI.....iv
UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU.....iv
MAONO.....v
TAMKO LA LENGO MAHUSUSI.....vi
LENGO KUU.....vi
DIBAJI.....vii

1.0: Kashfa..... 1
1.1: Maana ya Kashfa..... 1
1.2: Aina za Kashfa..... 1
1.2.1: Kashfa kwa Maandishi (libel)..... 1
1.2.2: Kashfa kwa Matamshi (Slander).... 2
2.0: Sheria Zitumikazo katika Kashfa..... 2
3.0: Mambo Muhimu ya Kuthibitisha Kashfa...2
3.1: Nia Mbaya.....2
3.2: Matamshi/Maandishi Lazima yawe ya Kashfa..... 3
3.3: Matamshi/Maandishi lazima yamlenge Mlalamikaji..... 3
3.4: Matamshi/Maandishi lazima Yaenezwe.....4

4.0: Utetezi..... 5
4.1: Kama anaweza Kuonyesha kuwa Matamshi au Maandishi ni ya kweli..... 5
4.2: Maoni yalitolewa kwa nia Njema... 5
4.3: Upendeleo (Privilege).....5
5.0: Fidia..... 6
5.1: Aina za Fidia..... 6
5.1.1: Fidia ya Jumla..... 6
5.1.2: Fidia ya Adhabu..... 7
5.1.3: Nyongeza ya Fidia..... 7

SHUKURANI

Tunatoa shukurani kwa wanasheria wetu na wale wa kujitolea katika uandaaji wa vijarida hivi. Pia tunawashukuru kwa dhati wale wote walioshiriki kwenye kukirejea kijitabu hiki ili kuandaa toleo hili la tatu hususan Wakili Harold Sungusia, Wakili Fulgence Massawe, Wakili Jeremiah Mtobesya, Bw. Rodrick Maro na Bw. Evans Sichalwe, pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiasa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania mnamo Septemba, 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET). Makao makuu ya Kituo ni Dar es Salaam na Arusha kuna ofisi ndogo.

MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina tamani jamii yenye haki na usawa.

TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibiashara linalojibidisha kukuza uwezo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa utakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa sheria.

DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina kazma ya kusaidia jamii ya watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pamoja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kuwa kwa raia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi tu ya sheria zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote kujua sheria. Hali hii inasababisha watu wengi kujikuta katika matatizo ya kisheria ambayo yangeweza kuepukika kama angejua sheria. Ndio maana basi Kituo kimeamua kutoa machapisho haya na mengine, kwa lengo la kutoa msaada wa kisheria kwa raia.

Huu ni usaidizi kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ya kisheria ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufumbuzi au maelekezo ya tatizo linalokusibu. Ni lengo letu kuwa, katika

vijitabu hivi tunatoa usaidizi wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapopata matatizo ya namna hii.

Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria au uende kwa mwanasheria aliye karibu na wewe ili aweze kukusaidia. Tunaamini utapata usaidizi huu kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia kwa karibu. Umalizapo, tafadhali umsaidie na mwenzako kupata usaidizi huu.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

1.0: Kashfa

1.1: Maana ya Kashfa

Kashfa ni kitendo cha mtu kutoa hadharani taarifa za uongo juu ya mtu mwingine. Habari hizo humshushia hadhi, katika jamii, mtu aliyetajwa kwenye habari hizo. Ili taarifa iwe ya kashfa ni lazima ilenge kujenga chuki, dhihaka na dharau kwa mtu yeyote atakayeyasikia, kuona.

Aidha kosa la kashfa limeainishwa katika sheria kwa lengo la kulinda heshima ya kila mtu sababu kila mtu ana haki ya kuthaminiwa utu wake.

1.2: Aina za Kashfa

Kuna aina mbili za kashfa:-

(i) Kashfa kwa njia ya maandishi;

(ii) Kashfa kwa njia ya matamshi.

1.2.1: Kashfa kwa Maandishi (*libel*)

Kashfa kwa njia maandishi ni ile inayowekwa katika hali ya kudumu na yenye kuonekana kama vile kuandika machapisho, kuonesha sinema au kuchora katuni, sanamu na kadhalika.

Hivyo kashfa ya maandishi ipo katika hali ya kudumu. Hii ni kwa sababu maandishi huifadhika.

1.2.2: Kashfa kwa Matamshi (*Slander*)

Hii ni aina nyingine ya kashfa. Kashfa kwa njia ya matamshi inafanywa kwa maneno ya kutamka au kwa njia ambazo zinasikika au kuonekana lazima zinalenga katika kumvunjia mtu heshima yake katika jamii.

2.0: Sheria Zitumikazo katika Kashfa

Kuna Sheria ya Magazeti 24 ya mwaka 1976 ambayo imeweka kanuni zinazohusika na mambo ya kashfa. Kwa mfano katika kifungu 157(1) cha sheria za magazeti kinaeleza kwamba wakati suala la kashfa likizungumzwa mahakamani lazima hakimu akae na wazee wa baraza.

Sehemu nyingine ya sheria ni maamuzi ya mahakama katika kesi za kashfa zilizokwisha amuliwa hapo awali (*case law*). Katika kesi hizo mahakama lazima ifuate katika kutoa haki.

3.0: Mambo Muhimu ya Kuthibitisha Kashfa

Ili mtu aliyekashfiwa aweze kushinda kesi yake, lazima athibitishe mambo yafuatayo:-

3.1: Nia Mbaya

Mlalamikaji lazima aoneshe kwamba kashfa iliyotolewa dhidi yake ilisambazwa kwa nia mbaya

bila kuwa na sababu za msingi kwa mfano, Juma ni mgombea safi wa ubunge lakini Hamisi kwa nia ovu, huku akijua si kweli, anatangaza kwamba Juma ni mla rushwa na hafai kuwa kiongozi. Hali hii inafanya Juma kukosa ubunge kutokana na wapiga kura kuamini maneno ya Hamisi. Katika hali kama hii ni wazi kwamba Hamisi amesema maneno hayo kwa nia mbaya ya kutaka Juma akose ubunge.

3.2: Matamshi/Maandishi Lazima yawe ya Kashfa

Ili mlalamikaji aweze kushinda kesi yake ni lazima aonyeshe kwamba matamshi au maandishi yalisababisha heshima yake kushuka kwa wanajamii na kufanya wanajamii kumdharau, kumkimbia na kumdhihaki. Matamshi au maandishi lazima yatolewe kwa njia ambayo mtu yeyote katika jamii anaelewa yamekusudia nini.

3.3: Matamshi/Maandishi lazima yamlenge Mlalamikaji

Mlalamikaji lazima aonyeshe kwamba matamshi au maandishi yaliyotolewa au kuchapishwa yalimlenga yeye na si vinginevyo. Kama ikithibitika hivyo, mlalamikiwa hataweza kudai kwamba matamshi au maandishi yaliyotolewa/kuchapishwa

hayakumlenga mlalamikaji. Ila kitu muhimu ni kwamba mwanajamii yeyote aliyesikia au kuona maandishi hayo anapeleka mawazo yake kuwa aliyelengwa si mwingine bali ni mlalamikaji. Hata hivyo kashfa haiwezi ikalenga kikundi cha watu, shirika au tabaka la watu fulani. Ili kuthibitisha kwa kosa la kashfa hiyo iwe imemlenga mtu binafsi na sio kikundi cha watu fulani.

3.4: Matamshi/Maandishi lazima Yaenezwe

Lazima maneno yaliyotolewa aidha kwa matamshi au kwa maandishi yawafikie watu wengine mbali na mlalamikaji. Kwa mfano iwapo "X" atatoa habari za uongo mbeleya "P" kwa kumkashifu kuwa ni mwizi "P" hataweza kupeleka dai hilo mahakamani kwa kudai "X" alimkashifu wakati kulikuwa hakuna watu wengine zaidi yao waliosikia au kuona.

Angalizo: Endapo kashfa ya maandishi au ya matamshi itarudiwa kwa nyakati tofauti tofauti basi kila rudio linahesabiwa kuwa ni kashfa inayojitegemea.

4.0: Utetezi

Wakati mwingine mlalamikiwa anaweza kukwepa adhabu kuwa alitoa kashfa kwa kujitetea kama ifuatayo:-

4.1: Kama anaweza Kuonyesha kuwa Matamshi au Maandishi ni ya Kweli

Mlalamikaji anaweza kujitetea kuwa yale aliyosema/kuandika ni ukweli mtupu hata kama baadhi ya maelezo yake si ya kweli. Hapa lazima mlalamikiwa aonyeshe kuwa aliyoyasema/ kuandika aliamini kuwa ni ya kweli. Kama ataweza kufanya hivyo basi hataonekana mwenye hatia.

4.2: Maoni yalitolewa kwa Nia Njema

Iwapo masuala yanayosemwa dhidi ya mlalamikaji ni maoni yaliyotolewa kwa nia njema yaani kwa manufaa ya umma basi mlalamikiwa anaweza kuonekana hana hatia. Aidha, suala la maslahi ya umma ni pana sana hivyo linahitaji busara ya Jaji/ hakimu anayesikiliza kesi ya aina hii kuamua nini kichukuliwe kuwa ni maslahi ya umma.

4.3: Upendeleo (*Privilege*)

Kuna baadhi ya matukio ambayo sheria kwa sababu mbalimbali imeyapa kinga ya upendeleo.

Hivyo basi baadhi ya mambo yanayosemwa au yatakayosemwa au kuandikwa yana upendeleo wa kinga kwamba hakuna hatua za kisheria zitachukuliwa kutokana na sera za umma.

5.0: Fidia

Kama ilivyoainishwa, kashfa inasababisha madhara katika heshima na hadhi ya mlalamikaji. Madhara haya yanaweza kugawanyika katika sehemu mbili:-

(i) Madhara ayapatayo mtu kutokana na ile hali ambayo jamii imemwelewa kutokana na yaliyosemwa au kuandikwa ambapo hadhi yake ilishushwa.

(ii) Kusononeka au chukizo lililosababishwa na kashfa iliyotolewa kwa mlalamikaji mwenyewe.

5.1: Aina za Fidia

Hivyo, mtu akipata madhara kama ilivyoelezwa hapo juu, mahakama inampa fidia inayotolewa kwa aina zifuatazo;

5.1.1: Fidia ya Jumla

Hii ni kiasi cha fedha ambacho mahakama inaamua mlalamikaji alipwe. Kiasi hicho hutolewa

kwa kutofuata kiasi alichoomba mlalamikaji. Hii inatokana na hali halisi kwamba mahakama huonelea kwamba si rahisi kupima thamani ya heshima na hadhi ya mtu kwa kiwango cha pesa.

5.1.2: Fidia ya Adhabu

Hii ni fidia inayotolewa na mahakama kama adhabu kwa mlalamikaji ikiwa ni nia ya mahakama kumlinda mlalamikaji, hasa pale ilipothibitika kwamba kashfa ilifanyika kwa nia mbaya juu ya mlalamikaji.

5.1.3: Nyongeza ya Fidia

Mahakama huweza kutoa nyongeza ya fidia kwa mlalamikaji kama kiasi cha pesa alichoomba kilikuwa kidogo ikilinganishwa na madhara aliyopata. Nyongeza hii huzingatia madhara yaliyosababishwa na kashfa.